Kwa Jina La Allaah, Mwingi wa Rehema, Mwenye Kurehemu

Al-Hudaa [Uongofu]

الهدى

25/= Ksh

Volume 8, Issue 4

20th Rabee ul-Aakhar 1432

25th March, 2011

Yaliyomo

SHEITANI NA NJIA ZAKE... 1 - 3

USIKATE TAMAA NA... 4

SHAITANI NA NJIA ZAKE ZA KUPOTOSHA WAUMINI

Mtayarishi: Sheikh 'Abdullah Al-Khater

1.MAUMBILE YAKE SHEITANI

Ni nani sheitani? Hili ni suala muhimu katika dini ya kiislamu. Baadhi ya watu waamini kuwa neno :sheitani: lamaanisha kila jambo ambalo mtu huweza kupagawa ; wengine wadai kumainisha ni viumbe vingi visivyo onekana maumbile yake kwa macho {microorganisms] vinavyo ishi pamoja nasi.Na wengine washikilia kuwa nikila ishara ya jambo baya.

Hata hivyo katika itikadi ya kiislamu sheitani ni mmoja katika jamii ya kijini ambao wako katika maubile na hali yao kivyao, wameumbwa na uwezo wakuweza kujificha na macho ya binadamu.Allaah (سبحانه وتعالى) asema kwenye Qur'an **[Na (kumbuka) pindi tuliposema (kuwaambia) Malaika, msujudieni Adam. Nawalisujudu isipokuwa Iblisi ambaye alikuwa nikatika majini (lakini daraja yake ilikuwa wakati huo nikama malaika), kwahivyo alivunja Amri ya Mola wake, basi je mumuabudu yeye na kizazi chake kwa asie kuwa mimi na ilhali (mashetani) wao ni maadui ; ubaya wa madhalimu kubadilisha (kwa kuwatii, mashetani nakumuasi Allaah)].(kahf 18) 50]**

Sisi Waislamu twaamini kuweko kwa majini pamoja na iblisi (sheitani) na kulinngana na hadithi ya Mtume (صلى الله عليه وسلم) **[kila mtu ana mshirika wake kutoka miongoni mwa majini na mshirika kutoka miongoni mwa malaika]. Dalili hii yapatika kutoka vivile kwenye sura ya Qur'an [Sema, najilinda kwa Muumba wa watu. Mfalme wa watu. Mola wa watu. Nashari ya anaye tia wasiwasi anaye regea nyuma. Atiaye wasiwasi nyoyoni mwa watu. Miongoni mwa majini na wanaadamu. (An-Naas114):1-6)]**

Vile vile sheitani aongezeka idadi yake (kama vile wanavyo ongezeka wanaadamu) kwani naye ana kizazi chake. Asema Allaah (سبحانه وتعالى) kwenye Qur,an [**Na(kumbuka)pindi tuliposema (kuwaambia)Malaika, msujudieni Adam. Nawalisujudia isipokuwa Iblisi ambaye alikuwa nikatika majini (lakini daraja yake ilikuwa wakati huo nikama malaika), kwahivyo alivunja Amri ya Mola wake, basi je mumuabudu yeye na kizazi chake kwa asie kuwa mimi na ilhali (mashetani) wao ni maadui ; ubaya wa madhalimu kubadilisha (kwa kuwatii, mashetani nakumuasi Allaah)].(kahf 18) 50]**

Kwa njia hii sheita na kizazi chake na wafuasi wao wafanya juhudi kubwa ya kuwatia matamanio watu na kuwapoteza katika maisha yao.

2.SHEITANI KUMNYEMELEYA MWANA-ADAMU

Sheitani yuwamnyemelea mwanaadam kwakutumia njia za siri kabisa. Lengo lake kubwa likiwa ni kumpoteza akitumai mwisho wake atakuwa kafiri au kwa uchache amtie kwenye ushirikina. Lakini wakiwa imara nawakawa wameshika kamba ya ALLAAH (سبحانه وتعالى) kwa nguvu hutumia njia nyingine akenda kuwatamanisha waumini wakikweli wazushe na kutoa fatwa za kigeni kinyume na uislamu wa kikweli. Ikiwa bado wako imara basi anajaribu

SHAITANI NA NJIA ZAKE ZA KUPOTOSHA WAUMINI

kuwafanya watende dhambi kubwa. Na akiona kuwa waumini hawatafanya madhambi makubwa sheitani havunjiki moyo yuanza kumpambia yale madhambi ambao wengi wayaona ni madogo nayo nikule kuwafanya washughulike namambo ya upuuzi. Mwisho juhudi ya sheitani ikija kuingia kitotoro cha giza anajaribu kufanya mambo ya halali yenye kuhimizwa yaonekane kuwa ni yenye kuvutia kuliko yale ambayo ni ya wajibu katika maamrisho.

Katika juhudi yake yakumpoteza mwanaadam na kutumia udhaifu wake sheitani anao mwenendo na utaratibu maalum ambao Allaah (سبحانه وتعالى) ametuonya nao kweye Qur,an [**Nawala msizifuate hatua za sheitani hapana shaka ya sheitani kwenu ni adui aliye wazi. (al-Anaam 6):142**]

Vile shetwani anavyo wanyemelea binaadam ni tafauti kwa kila mtu, hufuata matamanio na mapenzi yao makubwa. Atumia uchaji Mungu kuwashambulia wachaji Mungu; adabu za kielimu kuwashambulia wavyuoni; na ujinga kuwashambulia wajinga.

3.NJIA ZA SHEITANI KATIKA KUMPOTEZA MWANAADAMU

Shaitani huondosha umakinifu na kutia shaka kwenye nyoyo za waislamu.Hivyo kusababisha wathaniane vibaya. Mtume (صلى الله عليه وسلم) yuwahadithiwa yakuwa alisema [**shaitani amekata tamaa yakuabudiwa na waja wema lakini atafuta kuwachochea baina yao**]. Tuhuma na shaka mara zote huelekeza mtu kuwa na fikira mbovu, haswa ikiwa nimshindo wa ushawishi wa sheitani kwenye moyo wa mtu.:Ummu al-Mu'mineen Safiyya bint Huyey (رضي الله عنها) alihadithia kuwa [**siku moja usiku wakati Mtume (صلى الله عليه وسلم) akijipumzisha msikitini kwa ajili ya ibada nilimwendea. Tukazungumza kisha nikataka kurudi nyumbani. Akasimama kutaka kunisindikiza. Tukawa twatembea bega kwa bega kwenye giza watu wawili wakatuona na wakamtabua Mtume (صلى الله عليه وسلم) wakaanza kutembea kwa haraka wanavyo weza, lakini Mtume (صلى الله عليه وسلم) akawasimamisha akasema: "ngojeni enyi watu wawili, huyu ni Safiyya bint Huyey; wale watu wawili wakasema :subhana Allaah, ewe Mtume wa Allaah; Yeye Mtume (صلى الله عليه وسلم) akaongeza kusema:"hakika sheitan atembea kwenye kiwiwili cha mwanaadamu kama damu inavyo tembea kwenye mishipa na huenda akawa imetia kwenye fikira zenu mawazo mabaya"].**

Mwamke atembea bega kwabega na mwanamume usiku, hali ambayo yaweza kusababisha mtu kuleta uamuzi waharaka. Lakini Mtume (صلى الله عليه وسلم) akataka kujieleza nakuondosha shaka na dhana mbovu ambayo huenda ikawa imewagusa watu wawili wale na kwahivyo Mtume (صلى الله عليه وسلم) akawazuia na kuwaeleza kuwa alikuwa akimsindikiza mkewe nyumbani.

Hili ni somo ambalo sote twafaa kujifunza. Tusiache jambo lashaka bila ya kulifafanua ili isipatikane nafasi yakupikwa huja nakuenezwa kwa habari.

Sheitani vilevile achochea watu kuteta akawajaza hisia za uadui. Sulayman ibn Al-sar'd (رضي الله عنه) alihadithia akisema, [**nilikuwa nimekaa na Mtume (صلى الله عليه وسلم) tukasikia watu wawili wakiitana majina mabaya (wakitukanana). Mtume (صلى الله عليه وسلم) akasema najua dua ambayo ikitamkwa yaweza kufukuza hasira zao. Hii nikusema(AUDHU BILAHI MINA SHEITWANI AR-RAJEEM) najilinda kwa Allaah na sheitan aliye laaniwa**]

Baadhi ya mipango ya sheitani ni kumsukuma Muumini kufanya mambo kupita kiasi. aidha kupuuza jambo bila kujali au kuwa na hamu ya kupita mipaka. Akiona yakuwa shabaha yake ni sampuli ya mtu atafutae vipengele au udhuru yuwamuhudumikia kwa jambo hilo. Humbandika uvivu na ajizi.

Yuwamfungulia mlango wakutii tafsiri na amri za upotofu. Apatia vitendo vibaya majina ya kupendeza ili awavutie wale ambao waweza kwa urahisi kuathiriwa. Kwa njia hii alewesha wahasiriwa wake akawafanya waamini mambo yalio katazwa kuwa niya halali.

Na akiona kuwa shabaha yake ana bidii ya kutekeleza wajibu wake katika dini anajaribu kumhakikishia kuwa afanye juhudi zaidi.

Amhakikishia yakuwa matendo anayo yatenda(mazuri) hayatoshi na kwamba ikiwa tamaa yake nikuwa mtukufu nilazima awe na juhudi kuliko wengine. Asilale wengine wakifanya hivyo; asivunje saumu yake wakati uliowekwa; ikiwa wengine waosha nyuso zao na mikono mara tatu wakati wanapotawadha, basi yeye aoshe uso na mikono yake mara saba nakadhalika.

Kuna wale wanaofanya madhambi, lakini waswali swala zao tano kila siku.Waamini kwa vile wao watekeleza nguzo kubwa kwenye uislamu ambayo ndio itakayo tizamwa mwamzo siku ya hisabu, kwa hivyo hakuna ubaya tukifanya baadhi ya madhambi wakitaraji yakuwa madhambi hayo yaweza kusamehewa.

Kuna wengine wanaosema kuwa dini ya uhakika inadhihirishwa kwenye adabu nzuri na tabia njema kwa watu. Kwao wao ni muhimu zaidi kuwa wema kwa watu nakuwahurumia kuliko kutekeleza wajibu wao wakufanya amali walizo amrishwa na Allaah (سبحانه وتعالى) na Mtume wake (صلى الله عليه وسلم).

Vile vile ni muhimu kwao zaidi kuwa na nia nzuri moyoni kuliko kutekeleza kwao vitendo.

Kuahirisha au kuchelewesha mambo mpaka baadae nikatika njia ambayo yatumiwa na sheitani anaponyemelea wahasiriwa wake. Awawekea vizuizi au vizuizi hutokeza njiani mwao ili

(Endelea kwenye Ukurasa wa 3)

SHAITANI NA NJIA ZAKE ZA KUPOTOSHA WAUMINI

(Endelea kutoka Ukurasa wa 2)

awafanye wakatize nyadhifa nawajibu wao kwenye dini mara moja. Kwa mfano mtu huenda akasema nitarejea kwa Allaah niombe toba, lakini nikimaliza masomo au nikipata kazi.

Wakati mtu anapo jihisi kuwa yeye yuko sawa sawa kabisa au yeye ni bora mno kuliko wengine hili kwa hakika nihisia mbaya ambayo sheitani amemtia kwenye moyo wake. Jambo hili humfikisha mtu kuanza kujisifu nakujitukuza. Mtu aliye dhurika na hili mara nyingi atizama watu kwajicho la dharau. Mtu kama huyu Abadan hawezi kukubali kuwa aweza kufanya makosa. Kila mara nimeona mtu waaina hii huacha kujifunza pindi afanyapo kosa dogo, hasa ikiwa nikatika doria ambayo Qur'an yasomeshwa. Badala ya kuhudhuria duroos hizi kila siku ili ajaribu kurekebisha makosa yake haji kabisaa, kuondosha kuonekana kuwa hajui nakujisalimu na izara, kwa hivyo hamalizi lile alilo lianza

Asipofaulu sheitanl kuchemsha fahari nakiburi cha mtu ,anajaribu kumshawishi awe mnyenyekevu, Huendelea kumshawishi kwenye fikra yake kuwa yeye hana uwezo wa kufanya lile analo panga kulifanya, hilo ni jambo lilo wekewa watu maalum wewe huliwezi. Hili husababisha mtu kujiteremsha daraja , wakati mtu aliye dhurika, aanza kujidharau, kujitukana na kujihisabu dhaifu kwenye uwezo wake; kwahivyo ayakinishiwa kuwa yeye kila mara ni mkosa.

Katika njia mbovu nakali anayotumia sheitan kuwapotosha wahasiriwa wake awafanya wawe na shaka ya yale wanayo yaamini. Akigundua kuwa mtu aandama njia iliyo nyoka, kwa hivyo akawa ashikamana na amri za Allaah (سبحانه وتعالى), anajaribu kumfanya shabaha wake awe na shaka kuweko ukweli wa yale anayo yatenda. Na kwavile wengi wa watu si waumini waki kweli huwashawishi huku akishangaa ikiwa wote watakwenda motoni.

Mizani hapa si tabia inayo zingatiwa na wengi au kidogo.Tabia njema hata hivyo ni kutenda lililo la sawa mbele ya Allaah (سبحانه وتعالى) na Mtume wake (صلى الله عليه وسلم). Asema Allaah (سبحانه وتعالى) kwenye Qur'an [**na hawakuwa wengi wa watu ni wenye kuamini na lao hata wafanya pupa (yusuf 12):103**].

Na'eem ibn Hammad yahadithiwa kuwa alisema [**"kundi la waislamu laweza kuunda ummah mmoja ikiwa wataonyesha imani ya yakini na twaa kwa Allaah** (سبحانه وتعالى)**. Lakini kundi hilo likipotoka na kuwa wapotofu mtu atakiwa ayashike imara yale ambayo walikuwa wakiyatenda wakati wakitenda mema kwa yakini; na akiwachwa peke yake huku akifanya juhudi ya kuhifadhi imani yake yeye peke yake aunda umma kwa sababu Allaah** (سبحانه وتعالى) **yuko nae.**]

Silaha nyingine inayotumiwa na sheitani ni ile ya khofu. Anajaribu kuwatisha waumini kuwa watadhuriwa na wafuasi na wasaidizi wake. Allaah (سبحانه وتعالى) asema kwenye Qur'an [**hapana shaka ni sheitani anayewaogopesha marafiki zake(makafiri) basi msiwaogope naniogopeni mimi ikiwa kweli ni wenye kuamini (Al-IMRAN 3):175**]

Allaah (سبحانه وتعالى) asema kwenye Qur'an [**sheitani yuwawakhofisha na ufakiri(mtakapo toa sadaka)na kuwaamrisha kufanya(mambo) machafu. Na Allaah yuwawaahidi msamaha(wamadhambi yenu mtakapo toa mali yenu katika njia yake) nakupewa badali ya mlichokitoa kwa njia ya ziada. Na Allaah ni mweye wasaa Mjuzi (al-Baqaraa2):268**] .Kwa hivyo mtu huenda akaiambia nafsi yake kuna bahati gani ya kupata kazi ya halali ikiwa nita iwacha kazi hii ya haramu ninayo ifanya sasa? Lakini, Allaah (سبحانه وتعالى) asema kwenye Qur'an [**na anayemcha Allaah atamfanyia (Allaah) katika jambo lake, (tatizo) matokeo. Na atamruzuku kwa namna asioyoitarajia. (At talaq -65):2-3**]

Hilo pia lawahusu wale wanao shughulika na mali ya riba. Wanadai kuwa watu tunaoishi nao watajirika kila siku kwahivyo nao ni lazima wawe sambamba na wenzao kwa namna yoyote. Kwa njia hii uovu wavishwa majoho ya kukopa kuficha ukweli wa mambo.

4-ATHARI ZINAZO FANYA KAZI YA SHEITANI RAHISI

A-Ujinga: nivigumu mno kwa sheitani kunyemelea wale wanao jishughulisha na elimu ya dini.

B-Kutokuwa na imani na twaa: Allaah (سبحانه وتعالى) asema kwenye Qur'an [**Alisema (Iblisi) ;basi naapa kwa utukufu wako, nitawapoteza wote. Isipokuwa waja wako katika wao uliowachagua (saad-38):82-83**]

C-Kutokuwa na hadhari na njia za sheitan.

5-TIBA AU DAWA

Wakati ijulikanapo sababu ya madhara tiba huwa ni yenye kuwezekana.

1-kumuamini Allaah (سبحانه وتعالى): Allaah (سبحانه وتعالى) asema kwenye Qur'an [**Hapana shaka hana uwezo wowote kwa walio amini na kwa Mola wao wategemea (An-Nahl 16):99**].

2-kutafuta ilmu ya kiislamu kutoka misingi iliyo ya sawa.

3-kujilinda na Allaah (سبحانه وتعالى) na kujistiri kwenye hema lake: Allaah (سبحانه وتعالى) asema kwenye Quran [**Nai ma akikushawishi sheitani kwa kukutia wasiwasi katika haki (ingawa anaaambiwa Mtume (صلى الله عليه وسلم) lakini makusudio ni wafuasi wake),basi jikinge kwa Allaah.Hapana shaka Allaah ni mwenye kusikia Mjuzi. (Al AaRAAF-7):200**] Hili laweza kutekelezwa kwa kusoma SOORAT –**AL FALAQ NA AN -NAAS**

USIKATE TAMAA NA MOLA WAKO: Sheikh Bakr Abu Zayd

Jipambe nafsi yako, ndugu yangu Muislamu, kwa ndani na nje kwa kumcha Allaah (سبحانه وتعالى): Usidharau hukmu za kisheria za Uislamu na uwe ni mwenye kuhakikisha na kuihuisha Sunnah kwa kuitekeleza pamoja na kuwahimiza wengine wazitekeleze (hizo Sunnah). Kuwa ni mwenye kuwalingania wenzako katika njia ya Allaah kwa kutumia ujuzi wa 'ilmu (ya dini) uliyo nayo, usuhuba wako kwao na kazi unayoifanya.

Jipambe nafsi yako kwa sifa za ushujaa, na moyo wa subra na muelekeo mwema. Msingi wa sifa hizi ni uchaji Mungu. Ni kutokana na sababu hiyo ndipo Imaam Ahmad (رحمه الله) aliposema: "Asili ya ilimu ni uchaji Mungu."

Kwahivyo jilazimishe juu ya uchaji Mungu kwa siri na kwa dhahiri. Watu bora ni wale wenye kumcha Allaah, na hakuna isipokuwa aliyesoma ndiye mwenye kumcha Allaah ipasavyo. Kwahiyo, wasomi ndiwo watu bora. Ukumbuke daima yakwamba hakuna msomi anaezingatiwa kuwa ni msomi wa kweli mpaka awajibike ipasavyo kuhusiana na aliyoyasoma, na hapana msomi awezae kuyatekeleza aliyoyasoma mpaka awe ni mcha Mungu.

Al-Khateeb al-Baghdaadee amenukuu maneno aliyoyaona, tena yenye mfano wa kustaajabisha, ambamo *mababa tisa* wamenukuliwa. Akasema: "Abul-Faraj, mwanae Abdul Wahhab, mwanae Abdul-Azeez, mwanae al-Haarith, mwanae Asad, mwanae al-Layth, mwanae Suleiman, mwanae al-Aswad, mwanae Sufyaan, mwanae Zayd, mwanae Ukainah, mwanae Abdullah at-Tamimi, alimnukuu babake aliyemnukuu babake mpaka kufikia babake wa tisa akisema, "Nimemsikiya Ali Bin Abee Twaalib akisema, "'Amali hutengenea kwa ilimu. Itengeneapo 'amali, hilo ni sahali; lakini kinyume chake ilimu hupotea." Maneno kama hayo vilevile yamenukuliwa kutoka kwa

NENO LA BUSARA

"Ukosefu wa adabu ndiyo sababu ya kila Shari."

'Ali Ibn Abee Twaalib [*Mu'jam Hikma tul 'Arab*]



NI KINA NANI JAMAA'AH

Ikapokewa na at-Tirmidhee kutoka kwa ibn 'Abbaas (رضي الله عنه) aliesema: Amesema Mtume (صلى الله عليه وسلم): **"Kwa hakika Allaah hawajumuishi Ummah wangu juu ya Upotofu, na Mkono wa Allaah uko pamoja na Jamaa'ah, na mwenye kujitenga na jamaa'ah ataingia motoni"** Jamaa'ah iliyokusudiwa katika hadeeth hiyo ni jamaa'ah ya wanavyuoni wakubwa waliofikia daraja ya ijtihaad. Yeyote anaejitenga na mfumo walioji-egemeza nao ma-'Ulamaa' basi atakufa mauti ya Jaahiliyyah kwa sababu jamaa'ah ya Allaah ni ma-'Ulamaa'. Allaah (سبحانه وتعالى) amewateuwa wao kuwa ni hujja kwa watu wote na wao ndiwo waliokusudiwa katika matamshi yake Mtume (صلى الله عليه وسلم) aliposema: "Allaah hawajumuishi Ummah wangu juu ya Upotofu". Na hiyo ni kwa sababu watu wa kawaida huichukuwa Dini yao kutoka kwao na kuwakimbilia wao pindi itokeapo mikasa na wakawafuata katika njia yao. Kwahivyo maana ya maneno ya Mtume (صلى الله عليه وسلم): "Ummah wangu hautojumuishwa", ni **"ma-'Ulamaa' wa Ummah wangu hawatojumuishwa juu ya upotofu".** Miongoni mwa waliosema maneno hayo ni 'Abdullaah bin al-Mubaarak na Is-haaq bin Raahawayy na kikundi cha ma-Salaf na ndio rai ya ma-'Ulamaa' wa Usool. Aliulizwa Abdullah bin al-Mubaarak: **"Ni nani hao jamaa'ah ambao watu wanatakikaniwa wawafuate?"** Akajibu, **"Abu-Bakr na 'Umar"**, - na akaendelea kuwataja wengine mpaka akafikilia kumtaja Muhammad ibn Thaabit na Hussein bin Waaqid - Akaambiwa: **"Hao (yaani: wote uliowataja) wameshakufa zamani, Jee, kuna wowote walio hai?"** Nae akajibu: **"Abu-Hamzah as-Sukkaree** - [Nae ni Muhammad ibn Maimoon Abu-Hamzah as-Sukkaree al-Mirwazee. Kulingana na tareekh, alikuwa ni muaminifu anaeheshimiwa na alikuwa ni Sheikh wa nchi yake (ibn al-Mubaarak) katika ilimu ya hadeeth. Alikuwa ni mfano ulio hai wa "Utu-mwema". Alikuwa akiwakirimu mno wageni wake mpaka akafikia kiwango kilichopita ukarimu wake kwao. Aliitwa as-Sukkaree kutokana na utamu wa maneno yake.]